BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Nne – Tarehe 24 Septemba, 2018.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

104. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:

Pamoja na jitihada kubwa za Serikali yetu kupeleka misaada katika Kaya maskini ili kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi, kumekuwa na tatizo la watu wachache kufaidika na misaada hiyo kila inapotolewa katika Kaya hizo.

(a) Je, Serikali inatumia vigezo gani katika kuwapa misaada watu hao kwa hao.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuwabadilishia maskini wengine kila muda ili nawao kuwapunguzia ugumu wa maisha kwa kupata misaada kama hiyo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

72. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Muda mrefu Serikali imekuwa ikitoa ahadi ndani ya Baraza hili kuhusu ukarabati wa kituo cha Afya cha Kitogani lakini hadi hivi sasa ahadi hiyo bado haijatekelezwa. Kwa vile hivi sasa Kituo hicho kipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini baada ya Ugatuzi. Ni matumaini ya wanachi wa Kitogani kituo hicho kitafanyiwa ukarabati mkubwa kwa haraka.

Je, ni lini hatua za ukarabati zitaanza ili wananchi wa Kitogani wapate huduma za afya katika mazingira mazuri.

77. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Njia ya viwanja vya Malindi iliyokuwa ya wapita kwa miguu ambayo kwa muda mrefu hivi sasa imefanywa maegesho na kuwekwa kifusi, ambacho siku za jua kinaleta vumbi jingi na siku za mvua kinasababisha tope na madimbwi ya maji hali, inayoleta usumbufu kwa watumiaji wa njia hiyo na wakaazi wa jirani.

(a) Kwa vile njia hiyo imefanywa maegesho ya gari na fedha zinakusanywa, Je, kwanini haijengwi kwa kiwango cha lami.

(b) Je, hatua gani zitachukuliwa kuondoa hali ya vumbi wakati wa jua na tope pamoja na madimbwi ya maji wakati wa mvua.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

64. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Sheria Namba 2 ya 2011 na kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 kifungu 68 hadi 70 imeanzisha chombo cha majadiliano ya pamoja katika Sekta ya Umma. Pamoja na kuundwa kwa chombo hicho mwaka 2015 hadi sasa hakijaanza kazi zake.

(a) Je, kuna sababu gani zinazofanya chombo hicho kisifanye shughuli zake.

(b) Je, Wizara yako haioni kwamba malalamiko mengi ya wafanyakazi yanatokana na kutokufanya kazi kwa chombo hicho kilichoundwa rasmi kupunguza malalamiko na kuharakisha upatikanaji wa haki katika Sekta ya Umma.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

48. MHESHIMIWA KHADIJA OMAR KIBANO (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa nia njema Serikali katika sera ya elimu imeanzisha elimu ya msingi ambayo kwa sasa ni lazima shehia ifunguwe madarasa ya maandalizi kupitia mradi wa (TUTU) tucheze na tujifunze.

(a) Je, Serikali imewaelekeza masheha kuandaa rasmi madarasa hayo ya maandalizi.

(b) Je, watoto hao wanasoma katika mazingira mazuri katika madarasa ya Qur-an.

(c) Je, Serikali haioni kuwa posho wanalopewa walimu hao halitoshelezi hata kima cha chini cha mshahara hakifikiwi.

Wizara ya Biashara na Viwanda

12. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Bishara na Viwanda:

Katika miaka ya nyuma zao la pili pili hoho Zanzibar lilikuwa linafanya vizuri katika mazao ya biashara, lakini hivi sasa zao hilo limepotea wala halitajwi.

Je, kwanini zao hilo limepoteza hadhi ya kuwa miongoni mwa mazao ya biashara yenye tija.

Wizara ya Afya:

41. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na tiba asilia ambazo hufikia kutangazwa kwenye magazeti na mabango. Hata hivyo, baadhi ya dawa hizo hukosa viwango vya kutibu wagonjwa na kuleta madhara na hata kusababisha vifo na nyengine hufanywa bila ya kufuata maadili.

(a) Je, tiba asilia ni halali Kisheria kutibu wagonjwa.

(b) Je, kweli au si kweli kuwa kuna tiba asilia ambazo zinapewa leseni kuendeleza huduma hizo.

(c) Kama hawana Sheria ya kutibu, ni nini hukumu ya mtoa huduma hiyo akikamatwa.

Wizara ya Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

151. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Mchezo wa mpira wa miguu unapendwa sana na vijana hapa nchini na ulimwenguni kwa jumla. Pamoja na kupendwa mchezo huo lakini pia ni sehemu ya ajira kwa wachezaji.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri ni wachezaji wangapi wa Zanzibar wanaochezea Ligi Kuu Tanzania Bara.

(b) Ni vilabu gani wanavyochezea wachezaji hao.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

150. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kanisa la Mkunazini waliomba kwa muda mrefu sana kwa Kamisheni ya Ardhi kuwa wana eneo lao wanataka kupimiwa kwa kuandika barua rasmi na nakala yake imepelekwa kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika na ardhi lakini mpaka leo hii hakuna kinachoendelea.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea mpaka leo hii eneo lao kutopimwa.

(b) Je, ni lini eneo lao hilo litapimwa ili wapate haki yao ya msingi.

(c) Je, Kamisheni ya Ardhi haioni imeshindwa majukumu yake ya kuwatumikia wananchi.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
24 Septemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.